

TAARIFA MAALUM KUHUSU HALI YA MAFUTA ZANZIBAR

ZURA inapenda kuwatoa khofu Wananchi kuhusiana na uvumi unaosambaa Nchini hasa kupitia Mitandao ya Kijamii kuwa kuna uwezekano wa kutokea 'Uhaba wa Mafuta' hapa Zanzibar.

Khofu hiyo imetokana na ukweli kwamba Meli ya 'United Spirit' ya Kampuni ya United Petroleum (UP) imechelewa kupakia Mafuta ya Petrol katika Bandari ya Dar es salaam, hata hivyo Meli hiyo inatarajiwa kufika Zanzibar siku ya Jumatano Tarehe 14/02/2018.

Kutokana na hali hiyo, kampuni ya United Petroleum (UP) kwa sasa haina mafuta ya petrol lakini mazungumzo ya ndani yamefanywa ili Zanzibar Petroleum (ZP) na GAPCO waweze kuipatia Mafuta Kampuni ya United Petroleum (UP) ili kuhakikisha Vituo vinavyomilikiwa na kampuni hiyo vinauza mafuta katika hali ya kawaida na kukidhi mahitaji ya Wananchi wa Zanzibar.

ZURA inasisitiza kuwa kuna Mafuta ya kutosha Nchini kwa bidhaa zote za Petroli, Dizeli na Mafuta ya taa yanayoweza kutumika kwa zaidi ya wiki mbili, hivyo hakuna uwezekano wa kutokea 'Uhaba wa Mafuta' kwa hali yoyote kwa kipindi hiki na Mamlaka inafanya jitihada za kutosha kuhakikisha hali ya upatikanaji wa bidhaa muhimu za mafuta nchini inakua endelevu

Hali ya Mafuta iliyopo Nchini kwa sasa ni kama ifuatavyo:-

Kampuni ya GAPCO

- Petrol: Lita 1,776,898
- Diesel: Lita 1,059,978
- Kerosene: Lita 481,942